GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXXIII Nam. 7229 **05 Aprili, 2024** **Bei Shs.3,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO Ukurasa

Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar,
Nam. 2 ya 2005
Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar
(Fao la Kuumia Kazini)(Marekebisho) 145

SEHEMU YA SHERIA

Sheria zilizotajwa hapo chini zimetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Sheria

Nam. 34:- Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Fao la Kuumia Kazini) (Marekebisho)

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA KUUMIA KAZINI) (MAREKEBISHO)

MPANGILIO WA KANUNI

KANUNI: **MAELEZO:**

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Kusomwa.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjikia kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakla zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

SEHEMU YA PILI
VIFUNGU VYA MAREKEBISHO

3. Marekebisho ya kanuni ya 1.
4. Marekebisho ya kanuni ya 2.
5. Marekebisho ya kanuni ya 6.
6. Marekebisho ya kanuni ya 9.
7. Marekebisho ya kanuni ya 10.
8. Marekebisho ya kanuni ya 11.
9. Marekebisho ya kanuni ya 12.
10. Marekebisho ya kanuni ya 13.
11. Marekebisho ya kanuni ya 15.
12. Marekebisho ya kanuni ya 16.
13. Marekebisho ya kanuni ya 30.
14. Marekebisho ya kanuni ya 34.
15. Marekebisho ya kanuni ya 37
16. Marekebisho ya kanuni ya 41.
17. Marekebisho ya Kanuni ya 43.
18. Kuongeza kanuni mpya ya 45.

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA KUUMIA KAZINI) (MAREKEBISHO)

[Chini ya kifungu cha 44(1)]

KWA UWEZO niliopewa chini ya kifungu cha 44(1) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya 2005, **Mimi, DKT. SAADA MKUYA SALUM,** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar ninafanya marekebisho ya Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Fao la Kuumia Kazini), 2023 kama ifuatavyo:

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Fao la Kuumia Kazini) (Marekebisho), 2024 na zitaanza kutumika mara baada ya kuwekwa saini na Waziri na kutangazwa katika Gazeti Rasmi.

Kusomwa.

2. Kanuni hizi zitasomwa pamoja na Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Fao la Kuumia Kazini), 2023 ambazo katika Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni Mama.

SEHEMU YA PILI
KANUNI ZA MAREKEBISHO

Marekebisho ya kanuni ya 1.

3. Kanuni ya 1 ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa kuondoa neno "Mheshimiwa" katika kanuni hii.

Marekebisho ya kanuni ya 2.

4. Kanuni ya 2 ya Kanuni Mama inarekebishwa katika kanuni ndogo ya (1) kwa kuondoa neno "Zanzibar" katika kanuni hii.

Marekebisho ya kanuni ya 6.

5. Kanuni ya 6 ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa:

(a) kuingiza maneno "yaliyoainishwa katika kanuni hizi" baada ya neno "mafao" katika aya (a);

(b) kufuta aya ya (c);

(c) kuipa jina upya aya (d) kuwa aya ya (c).

Marekebisho ya kanuni ya 9.

6. Kanuni ya 9 ya Kanuni Mama inarekebishwa katika kanuni ndogo ya (2) kwa kuongeza aya mpya ya (g) na (h) kama ifuatavyo:

"(g) ajali imetokea kwa mfanyakazi wakati akiwa katika hali ya ulevi au matumizi ya dawa za kulevya;

"(h) ajali inahusiana na chombo cha moto ambapo mwanachama aliyeumia alikuwa anaendesha mwenyewe chombo hicho akiwa hana leseni halali ya udereva au chombo kilichohusika na ajali iliyopelekea kuumia kwake hakikuidhinishwa kutumika barabarani kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazohusika."

Marekebisho ya kanuni ya 11.

7. Kanuni ya 11 ya Kanuni Mama inarekebishwa:

(a) kwa kuongeza kanuni ndogo mpya ya (4) na (5) mara baada ya kanuni ndogo ya (3) kama ifuatavyo:

"(4) Kutakuwa na kiwango cha chini cha malipo ya fao la kupatwa na majeraha ya muda kitakacholipwa kwa mwanachama ambacho kitakuwa sawa na asilimia kumi ya kima cha chini cha mshahara wa Serikali kwa mwanachama ambaye kiwango cha fao la kupatwa na majeraha na ulemavu wa muda kilichokokotolewa ni chini ya asilimia kumi ya kima cha chini cha mshahara wa Serikali kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (3) ya kanuni hii.

(5) Kutakuwa na kiwango cha juu cha malipo ya fao la kupatwa na majeraha ya muda kitakacholipwa kwa mwanachama ambacho kitakuwa sawa au si zaidi ya kiasi cha Shilingi Milioni Sita za Kitanzania kwa mwanachama ambaye atastahiki kulipwa fao la kupatwa na majeraha na ulemavu wa muda lililokokotolewa chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (3) ya kanuni hii, ambao umedumu kwa muda unaofikia na usiozidi miezi arobaini na nane na ukokotoaji wa fao hili utazingatia na kutumia ukomo wa kipato ulioainishwa katika Sheria endapo pato la mwezi la mfanyakazi husika ni zaidi ya kiwango cha ukomo wa kipato kilichoainishwa katika Sheria."

(b) katika kanuni ndogo ya (4) kwa kufuta maneno "pato la mfanyakazi huyo litaamuliwa na Mkurugenzi Mwendeshaji kwa kuzingatia pato ambalo mfanyakazi alikuwa anapata kabla hajaondoka kazini" na kuweka badala yake maneno "pato la mfanyakazi huyo litakuwa pato ambalo mfanyakazi alikuwa anapata kabla hajaondoka kazini"; na

(c) kuipa nambari upya kanuni ndogo ya (4), (5) na (6) kuwa kanuni ndogo ya (6), (7) na (8).

Marekebisho ya kanuni ya 12.

8. Kanuni ya 12 ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa kuongeza kanuni ndogo ya (4) mpya mara baada ya kanuni ndogo ya (3) kama ifuatavyo:

"(4) Katika kukokotoa fao la ulemavu wa kudumu ambao haumzuii mfanyakazi kurejea kazini, ukokotoaji wa fao hili

utazingatia na kutumia ukomo wa kipato ulioainishwa katika Sheria iwapo pato la mwezi la mfanyakazi husika ni zaidi ya kiwango cha ukomo wa kipato kilichoainishwa katika Sheria."

9. Kanuni ya 13 ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa kuongeza kanuni ndogo ya (3) mpya mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo: Marekebisho ya kanuni ya 13.

"(3) Katika kukokotoa fao la ulemavu wa kudumu ambao unamzuia mfanyakazi kurejea kazini, ukokotoaji wa fao hili utazingatia na kutumia ukomo wa kipato ulioainishwa katika Sheria endapo pato la mfanyakazi la mwezi ni zaidi ya kiwango cha ukomo wa kipato kilichoainishwa katika Sheria."

10. Kanuni ya 15 ya Kanuni Mama inarekebishwa: Marekebisho ya kanuni ya 15.

(a) katika kanuni ndogo ya (2) kwa kufuta maneno "arobaini na nane" baina ya maneno "miezi" na "la" na kuweka badala yake maneno "Thelathini na Sita".

(b) kwa kuongeza kanuni ndogo ya (4) na (5) mpya kama ifuatavyo:

"(4) Kutakuwa na kiwango cha chini cha fao la kifo kwa mfanyakazi aliyefariki kutokana na kazi kitakacholipwa kwa wategemezi wa mwanachama ambacho kitakuwa sawa na kima cha chini cha mshahara wa Serikali kikizidishwa mara thelathini na sita na kiwango cha juu cha fao la kifo ambacho kitakuwa sawa na kima cha chini cha mshahara wa Serikali kikizidishwa mara sabini na mbili.

(5) Katika kukokotoa fao la kifo kwa mfanyakazi aliyefariki kutokana na kazi, ukokotoaji wa fao hili utazingatia na kutumia ukomo wa kipato ulioainishwa katika Sheria iwapo pato la mfanyakazi aliyefariki la mwezi ni zaidi ya kiwango cha ukomo wa kipato kilichoainishwa katika Sheria."

11. Kanuni ya 16 ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta kanuni ndogo ya (1) na kuweka badala yake kanuni ndogo ya (1) mpya kama ifuatavyo: Marekebisho ya kanuni ya 16.

"16.-(1) Skimu italipa fao la kuumia kazini kwa wanagenzi au wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo watakaopata ajali kazini au maradhi yatokanayo na kazi au kifo kinachotokana na kazi katika taasisi ambayo ni mwajiri mchangiaji wa Mfuko ambao wanalipwa mshahara au posho na michango imelipwa katika Mfuko kwa ajili ya fao la kuumia kazini."

12. Kanuni ya 30 ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa kuongeza kanuni ndogo ya (3) mpya mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo: Marekebisho ya kanuni ya 30.

"(3) Skimu haitalipa fao la kuumia kazini kwa maradhi yanayosadikiwa kuwa yanatokana na kazi iwapo maradhi hayo yatagundulika ndani ya kipindi cha miezi ishirini na nne kutoka siku ambayo mfanyakazi husika ameajiriwa katika taasisi husika au miezi ishirini na nne baada ya mfanyakazi kustaafu kazi."

Marekebisho ya kanuni ya 34.

13. Kanuni ya 34 ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa kuongeza kanuni ndogo ya (6) mpya mara baada ya kanuni ndogo ya (5) kama ifuatavyo:

"(5) Katika utekelezaji bora wa Kanuni hizi, Bodi itaandaa na kutoa miongozo mbalimbali ikiwemo Muongozo wa Tathmini ya Ulemavu unaotokana na kazi na Muongozo wa Tathmini ya Maradhi yatokanayo na kazi na Miongozo hiyo itatumiwa na Madaktari au Bodi ya Madaktari katika kufanya tathmini inayotakiwa kwa ajili ya malipo ya fao la kuumia kazini."

Marekebisho ya kanuni ya 37.

14. Kanuni ya 37 ya Kanuni Mama inarekebishwa katika kanuni ndogo ya (1) kwa kuongeza maneno "au maombi ya fao la kuumia kazini hayakufanyika miezi mitatu baada ya mfanyakazi kupona au kurudi kazini" baada ya neno "kifo".

Marekebisho ya kanuni ya 41.

15. Kanuni ya 41 ya Kanuni Mama inarekebishwa katika kanuni ndogo ya (1) kwa kufuta neno "moja" baina ya maneno "milioni" na "au" na kuweka badala yake neno "tano".

Marekebisho ya kanuni ya 43.

16. Kanuni ya 43 ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta kanuni ndogo ya (1) na kuweka badala yake kanuni ndogo ya (1) mpya kama ifuatavyo:

"**43.**-(1) Kila Mwajiri Mchangiaji wa Mfuko atasajiliwa na kufuata masharti ya Idara ya Afya na Usalama Kazini Zanzibar kwa waajiri wa Zanzibar na Cheti cha Usajili kutoka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa waajiri wa Tanzania Bara kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria inayohusika na mambo ya usalama na afya kazini."

ZIMETIWA saini tarehe 26 mwezi Machi, 2024.

(DKT. SAADA MKUYA SALUM)
WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO
ZANZIBAR.